

MAKAO MAKUU

Ghorofa ya 4, Jengo la PSSSF, Barabara ya Makole
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania

Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

Barua pepe: info@ewura.go.tz

Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

TANGAZO KWA UMMA

MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJI KUTOKA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA TUNDURU (TUNDURU WSSA) KWA MWAKA 2019/20 – 2021/22

Maombi ya Mabadiliko ya Bei Na. TR-W-18-050-2018/2019

Mnamo tarehe 17 Juni 2019 Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea maombi yaliyokamilika kutoka Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Tunduru (Tunduru WSSA) ya kutaka kurekebisha bei za huduma zake za maji safi kwa mwaka 2019/20 hadi 2021/22. Majedwali namba 1 hadi 4 hapa chini yanaonesha mchanganuo wa bei za sasa na bei zinazopendekezwa

Jedwali Na 1: Bei ya Sasa na Zinazopendekezwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi kwa Uniti moja ya ujazo)

Kundi la Wateja	Bei ya Sasa	Bei Zinazopendekezwa					
	2018/19	Mabadi liko	2019/20	Maba diliko	2020/21	Maba diliko	2021/22
Majumbani							
Kundi 1(0-5m ³)	540	141%	1,300	12%	1,450	3%	1,500
Kundi 2 (6-10m ³)	585	122%	1,300	12%	1,450	3%	1,500
Kundi 3 (>11m ³)	625	108%	1,300	12%	1,450	3%	1,500
Taasisi	550	173%	1,500	13%	1,700	18%	2,000
Biashara	605	231%	2,000	25%	2,500	8%	2,700
Viwanda	760	163%	2,000	25%	2,500	20%	3,000
Magati(Sh./lt.20)	20	100%	40	13%	45	11%	50

Jedwali Na 2: Bei ya Sasa na Zinazopendekezwa kwa Wateja Wasio na Dira (TZS kwa Mwezi)

Kundi la Wateja	Bei ya Sasa	Bei Zinazopendekezwa					
	2018/19	Mabadi liko	2019/20	Mabadi liko	2020/21	Mabadi liko	2021/22
Majumbani	4,500	111%	9,500	5%	10,000	10%	11,000
Taasisi	16,500	112%	35,000	29%	45,000	11%	50,000

Biashara	16,500	112%	35,000	29%	45,000	11%	50,000
Viwanda	16,500	24%	20,500	49%	30,500	33%	40,500

Jedwali Na 3: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Maunganisho Mapya ya Maji (Shilingi/ Maunganisho)

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa	Ada Inayopendekezwa		
	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
Majumbani	13,500	Asilimia 20 ya Gharama za Maunganisho Mapya		
Taasisi	13,500			
Biashara	13,500			
Viwanda	13,500			
Magati	13,500			

Jedwali Na 4: Ada ya Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma ya Maji (Shilingi/Marejesho)

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa	Ada Zinazopendekezwa					
	2018/19	Mabadi liko	2019/20	Mabadi liko	2020/21	Mabad iliko	2021/22
Majumbani	13,000	515%	80,000	0%	80,000	0%	80,000
Taasisi	13,000	515%	80,000	0%	80,000	0%	80,000
Biashara	13,000	1054%	150,000	0%	150,000	0%	150,000
Viwanda	13,000	1438%	200,000	0%	200,000	0%	200,000
Magati	13,000	515%	80,000	0%	80,000	0%	80,000

Kwa Mujibu wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Tunduru, sababu kuu za kuomba marekebisho ya bei za huduma zake ni gharama kubwa za uendeshaji na matenengezo, uhitaji wa fedha kugharamia ukarabati na ununuzi wa vifaa na kulipa tozo mbalimbali.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Jumatano, tarehe 14 Agosti 2019** katika **Ukumbi wa Klasta** uliopo Tunduru Mjini kuanzia saa **4:00 asubuhi**. Lengo la mkutano huo ni kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali, Baraza la Ushauri la watumia huduma zinazodhibitiwa na EWURA, wateja wa Mamlaka ya Maji Tunduru, na wananchi wote kwa ujumla kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyooneshwa hapo juu **ifikapo tarehe 21 Agosti 2019**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana katika ofisi za **EWURA KANDA YA NYANDA ZA JUU KUSINI, GHOROFA YA SITA, JENGO LA NHIF; MTAA WA KARUME, MBEYA** au **OFISI ZA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA TUNDURU**.

Imetolewa na:
Kaimu Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
(EWURA)
22 Julai 2019